

TAFSIRI MPYA ZA FASIHI YA KIRUSI KATIKA KISWAHILI

NELLI V. GROMOVA

Sehemu muhimu ya fasihi andishi ya Kiswahili yachukuliwa na fasihi iliyotafsiriwa kutoka lugha za kigeni. Inatosha kukumbusha tafsiri ya kidini iliyofanywa na wamisheni pamoja na tafsiri ya vitabu mbalimbali vya fasihi vya waandishi wa Ulaya iliyofanywa katika enzi ya kikoloni hasa ya kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Kwa mfano “Visa vya David Coperfield” [sic], “Robinson Crusoe kisiwani”, “Simba wa Tsavo” n.k. Ingawa vitabu vingi vilikuwa vimetafsiriwa na wageni, Waswahili walio maarufu walishugulika vile vile na kazi hiyo ya kufasiri kama wale Shaaban Robert anayehesabika kuwa mwanzilishi wa fasihi ya kisasa ya Kiswahili pamoja na rais wa kwanza wa Tanzania, baba wa taifa Mwalimu Julius Nyerere. Shaaban Robert alitafsiri katika Kiswahili mashairi ya Voltaire na Omar Khayam, Julius Nyerere alitafsiri kitabu cha Shakespeare Julius Caezar.

Baada ya Tanzania kujipatia uhuru fasihi andishi ya Kiswahili ilikuwa ikitajirika na tafsiri nyingi zaidi zikiwemo tafsiri za vitabu vya waaandishi mashuhuri wa Kiafrika, kwa mfano James Ngugi, Thomas Mofolo, Okot p’Bitek na wengineo. Fasihi ya aina hiyo imechangia kwa kiasi fulani katika kuikuza fasihi na utamaduni wa Kiswahili.

Aidha, vitabu vya fasihi ya Kirusi zilianza kutafsiriwa kuanzia miaka ya sabini karne iliyo-pita. Katika Soviet Union ilikuwa imeundwa idara maalum ya kuchapia vitabu iitwayo Progress (“Maendeleo”) ambayo ilishughulika na tafsiri ya fasihi ya Kirusi kwenda lugha za kigeni kikiwemo Kiswahili. Kwa kutojali kuwa sehemu kubwa zaidi ya tafsiri hizo zilikuwa ni tafsiri za maandishi yaliyoteuliwa ya Lenin, tena vitabu vingi vya kiitikadi, lakini kwa vyo vyote zilikuwa zimetafsiriwa pia riwaya “Dubrovskiy” (1987) ya Alexander Pushkin na “Mama” (1980) ya Maxim Gorky, riwaya na hadithi za waandishi wa kisasa kama wale Aleksey Tolstoy “Tabia ya mrusi” (1964), M. Sholokhov “Ajali ya mwanamume” (1962), G. Baklanov “Watabaki vijana milele” (1987), Nora Adamyan “Daktari wa kijiji cha milimani” (1963) na nyingi nyinginezo. Watafsiri wa vitabu hivyo walikuwa kama kawaida Waswahili waliokaa siku zile Moscow wakisomea taaluma fulani ama kufanya kazi redioni na katika idara hiyo ya kuchapia vitabu kwa lugha za kigeni (Husein Abdul-Razak, Herman Matemu, Ben Omburo na wengine). Halafu Warusi waliopata kuisomea Kiswahili na kuimudu kikamilifu walishiriki katika kazi hiyo ya kutafsiri, kwa mfano, mmoja wetu V. Makarenko alitafsiri “Historia ya dunia ya kale” (1988).

Baada ya Soviet Union kusambaratika shughuli hizo za kutafsiri fasihi ya Kirusi katika Kiswahili zilikuwa zimesimamishwa pamoja na kufungwa kwa idara zote zilizoshughulikia lugha na fasihi ya Kiswahili kama zile idara ya Progress, idara ya kuchapia kamusi iitwayo “Russkiy yazik” (yaani “Lugha ya Kirusi”), Redio Moscow na nyingine. Na hadi leo kwa bahati mbaya hazijafufuliwa. Lakini kwa bahati njema huko Tanzania kazi hiyo ya kutafsiri fasihi ya Kirusi ilianza miaka michache nyuma chini ya Kituo cha utamaduni cha Urusi na Tanzania. Mkurugenzi wa kituo hicho Rifat Pateev aliyehitimu kutoka Idara ya lugha za

Kiafrika ya Taasisi ya nchi za Asia na Afrika alianza kutoa tafsiri za vitabu vya Kirusi ndani ya mfululizo uitwao “Maktaba ya fasihi ya Kirusi”.

Kitabu cha kwanza kilichotolewa mwaka 1999 kilikuwa ni tamthilia ya mwandishi maarufu Nikolay Gogol iitwayo “Mkaguzi wa serikali”. Tamthilia hiyo ilionyeshwa jukwaaani katika Urusi kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1836 na baada ya hapo imetafsiriwa katika takriban lugha zote kuu za dunia. Tafsiri ya kwanza ya “Mkaguzi wa serikali” katika Kiswahili ilifanywa na Christian Mwakasaka na kuchapishwa mwaka 1979 huko Nairobi. Tafsiri ya pili ya mwaka 1999 imefanywa na Joshua Madumulla wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ile tafsiri ya kwanza ilitegemea tafsiri ya Kiingereza, ambayo ilifupisha matini asilia na kuigawa tamthilia ya Gogol kwa matendo mawili tu badala ya matano. Kwa upande wake, tafsiri ya pili pia ilifanywa kutoka kwenye tafsiri ya Kiingereza lakini kwa kuizingatia tamthilia ya Kirusi jinsi iliyotungwa na Gogol ikiwa na matendo matano, tena ilikuwa imehaririwa na mrusi.

Mwaka 2001 vilikuwa vimechapishwa vijitabu viwili vya mtunga mashairi maarufu wa Kirusi Alexander Pushkin. Cha kwanza kinaitwa “Hadithi ya Mfalme Saltan na mwanawe Guidon” ikiwemo “Hadithi ya Jogoo wa Dhahabu”. Cha pili ni “Hadithi ya Mvuvi na Samaki wa Dhahabu”, ambayo imetafsiriwa vilevile na J. Madumulla. “Hadithi ya mfalme Saltan na mwanawe Guidon” imetafsiriwa pia naye pamoja na Marcus J. Mbigili.¹

Kitabu kilichofuata mwaka 2002 kilikuwa ni mkusanyiko wa hadithi za kienyeji za Kirusi kwa jina “Dada Alyonushka na kaka Ivanushka” zikiwemo hadithi tatu yaani “Dada Alyonushka”, “Mrembo Vasilisa” na “Ivan wawili”. Hadithi zote tatu zilitafsiriwa na M. Mbigili.

Mwaka jana watafsiri wa Kiswahili walirudia tena maandishi ya Pushkin na kutafsiri riwaya yake fupi iitwayo “Postamasta”. Aliyetafsiri ni mwandishi wa kiTanzania Bernard Mapalala (ambaye riwaya yake ya kihistoria “Kwa heri Iselemagazi” imetolewa mwaka wa 1992).

Tafsiri hizo zote zilikuwa zimehaririwa na Mrusi anayeongoza kile Kituo cha Utamaduni Rifat Pateev, na bila shaka yoyote zinastahili sifa. Kwanza Watanzania waliweza kusikiliza tafsiri hizo kwa redio katika kipindi cha kila wiki kiiwacho “Kukumbuka Urusi”. Isitoshe, tamthilia “Mkaguzi wa serikali” na ile “Hadithi ya Mvuvi na Samaki wa Dhahabu” zilichezwa na kikundi cha waigizaji Watanzania na hata kuonyeshwa kwa televisheni.

Tafsiri hizo zote zinakubaliwa na kuthaminiwa na Watanzania wengi, hasa wale wataalam waliojifunza ama wanaojifunza sasa katika Urusi ambao walipata kujua lugha ya Kirusi na kusoma kwa Kirusi maandiko haya ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Wafasiri wa vitabu hivi walitumia lugha fasaha inayoeleweka na watu waliokusudiwa kupata ujumbe. Bila shaka, tafsiri hizi zinamfanya msomaji wake azidi kuwa na hamu ya kuzisoma.

Kwa upande mwingine, ukilinganisha tafsiri ya Kiswahili na matini asilia unaweza kuona kwamba mafanikio mengi yameonekana, lakini wakati ule ule matatizo kadha wa kadha yamejitokeza. Inaeleweka vizuri kwamba kutafsiri katika lugha ngeni yenye tipolojia tofauti, kanuni tofauti za fasihi, mfumo tofauti na karibu kila kitu tofauti ni kazi ngumu sana kupita

¹ Pia lilikuwa limetafsiriwa shairi moja “Prorok” (“Mbashiri”) la Pushkin ambalo lilisomwa na mwanafunzi wa kike toka Tanzania Anna Ismail Wire kwenye Shindano la kimataifa la lugha ya Kirusi lililofanyika mwaka uliopita mjini Moscow. Mwanafunzi huyu akawa mmoja kati ya washindi kumi.

kiasi. Tafsiri ni fani yenye kuhitaji ujuzi mzuri wa lugha mbili. Wafasiri Watanzania huwa wanafasiri kutoka Kirusi kwenda Kiswahili sio moja kwa moja bali kwa kupitia Kiingereza. Hivyo hitilafu ya tafsiri inaweza kueleweka na pengine kusameheka.

Kwa mfano, kwa maoni yangu kitu kilicho kigumu zaidi ni kutafsiri mashairi. Hadithi mbili za Pushkin vilitungwa kwa kanuni fulani za mashairi ya Kirusi. Yale mashairi ya “Hadithi ya Mvuvi na Samaki wa Dhahabu” hayana vina, ni mashairi huru (guni). Hivyo ilikuwa ni rahisi kuyatafsiri katika Kiswahili kwa sababu mashairi ya aina hiyo yapo katika lugha ya Kiswahili. Hadithi nyingine yaani “Hadithi ya mfalme Saltan na mwanawe Guidon” ilitungwa kwa mashairi yenye vina. Aina hiyo ya utunzaji wa mashairi hutumiwa sana na fasihi ya Kirusi: kila ubeti una mistari minne, mstari wake una urefu wa mizani minane (pengine saba), mwisho wa kila mstari kati ya miwili unafanana (maana silabi yao ya mwisho ni ile ile), tena mkazo huwa katika silabi ya kwanza, ya tatu, ya tano na ya saba:

Toly-ko vî-mol-vity us-pye-*la*,
Dvyery ti-hony-ko zas-kri-pye-*la*
I v- svyet-li-tsu vho-dit *tsary*
Sto-ro-nî toy go-su-*dary*

Mara tu alipowahi kusema,
Mlango uliatuka kidogo,
Na chumbani anaingia mfalme,
Aliye mkuu wa nchi hiyo.

Mashairi ya aina hiyo bila shaka sio rahisi kutafsiri katika lugha ya Kiswahili ambayo kanuni zake za utungaji mashairi ni tofauti kabisa. Ubeti niliotaja juu wenye mistari minne ilikuwa imetafsiriwa kwa mistari mitano:

Baada ya maneno hayo
Mlango wa chumba chao ulifunguka
Kwa kufanya mualiko mdogo
Na, tazama, mbele ya macho yao
Alisimama Mfalme wao.

Unaweza kuona au kusikia ya kuwa mashairi hayo hayana vina. Ni mashairi guni (blanc verse). J. Nyerere alipotafsiri mashairi ya Kiingereza alitumia sheria moja tu ya shairi la kawaida yaani kila mstari amejitahidi kufanya uwe na mizani 16, ingawa mistari hiyo haikuwa na vina wala haikugawanywa kwa beti. Kwa maoni yangu, ingewafaa watafsiri wa “Hadithi ya mfalme Saltan” wangejitahidi pia kutumia mizani ili kuonyesha tofauti kati ya hadithi hizo mbili za Pushkin zilizotungwa kwa mashairi yenye vina na mashairi yasiyo na vina.

Mara kwa mara inatokea kwamba mtafsiri anageuza kwa kiasi fulani ujumbe wa mwandishi mwenyewe. Katika hadithi juu ya mvuvi na samaki wa dhahabu mtungaji wake A. Pushkin aliandika juu ya mzee aliyekaa na mkewe baada ya kuoana miaka thelathini nyuma, maana yake mkewe alitimiza ama kukaribia umri wa miaka hamsini. Katika enzi la Pushkin umri wa kati wa maisha ya binadamu haukuzidi miaka 50! Hivyo mke wa mvuvi alikuwa

mzee sana na hakuweza kuwa “mzuri sana” kama Madumulla alivyotafsiri. Tena mke huyo eti mzuri “akamvamia mumewe kwa karipio”, “ukali wake ukazidisha”, “hajitambui kwa mahasira yaliyomzonga”, “akajibu mumewe kwa jeuri” – kwa maneno mengine, msomaji Mrusi na hata msomaji wa matini ya Kiswahili hawezi kukubali kwamba yule mwanamke mzee anahesabika awe mzuri. A.Pushkin anamwelezea kama “starukha” yaani bikizee ama ajuza. Hivyo inaonekana ya kuwa mfasiri hakuzielewa vizuri dhana alizozifasiri na kupotosha kidogo maana iliyoko katika lugha chasili.

Tena ni vigumu sana kutafsiri katika Kiswahili majina ya Kirusi yenye maana fulani. Katika tamthilia “Mkaguzi wa serikali” kuna wahusika wengi ambao majina yao yanasababisha msomaji Mrusi apate taswira ya tabia zao. Lile jina la konstabo “Dyerzhimorda” halina maana kwa msomaji wa Kiswahili: tafsiri yake sisizi ingekuwa kama “Shika uso mzito” (kwa Kirusi “morda” ni uso wa mnyama, na neno hili linatumika kwa ajili ya mtu ambaye unataka kumdharau). Ama lile jina la jaji “Lyapkin-Tyapkin” linatokana na mwigo “lyap-tyap”, maana yake ni kufanya kazi ovyo, bila nidhamu.

Aidha, majina ya wahusika wa hadithi “Dada Alyonushka na kaka Ivanushka” ni majina ya kitoto yanayoonyesha mapenzi ya mwandishi. Yamenyambuliwa kwa kiambishi-neemeshamaana -ushka, lakini msomaji wa tafsiri ya Kiswahili hawezi kuona tofauti kati ya majina ya kawaida ya Alyona na Ivan na majina yaliyoneemeshwa maana yake Alyonushka na Ivanushka.

Pengine ukilinganisha matini asilia na tafsiri yake unaweza kukuta maongezeko ya matini ya Kirusi katika tafsiri ya Kiswahili ama, kinyume chake, sehemu kadhaa za matini ya Kirusi zimeachwa pasipo kutafsiri. Niwatolee mifano miwili tu. Katika “Mkaguzi wa serikali” meya wa mji anamwuliza kamishina: “Umekuwa ukiwatoza wagonjwa kwa miaka 20, sivyo?”, lakini maneno hayo hayamo katika matini asilia ya Kirusi ya tamthilia hiyo.

Mfano mwingine, unaodhihirisha kuwa matini asilia ya Kirusi imepunguzwa katika lugha lengwa ya Kiswahili, unatokana na “Hadithi ya mfalme wa Saltan na mwanawe Guidon”:

Malkia wako usiku uliopita

Alizaa kiroja, si mwana, si binti

Wala hatujapata kuona mfanowe.

Matini ya Kirusi ya ubeti huu wenye mistari mine (sio mitatu iliyomo katika tafsiri) inatoa maelezo kamili juu ya kiroja hiki: “si mwana, si binti, si mtoto wa panya, si mwana wa chura, bali ni mwanamnyama asiyejulikana”.

Lazima nijisimamishe hapa kwa sababu mifano ya aina hiyo ningeweza kuitoa mingi zaidi. Wala sote tunajua ya kuwa ni rahisi kukosoa tafsiri ilivyo kuliko kufanya kazi hiyo ya kutafsiri mwenyewe. Kila mtafsiri ana staili yake pekee ya kutafsiri: ikiwa wafasiri wawili watapewa kutafsiri matini ile ile, bila shaka tafsiri zao mbili zitatofautiana kwa kiasi.

Kwa kumalizia inafaa kusema kwamba kwa jumla lugha fasaha ya tafsiri hizo mpya za fasihi ya Kirusi zinastahili sifa kubwa, tena ni mafanikio makubwa ya wafasiri Waswahili. Makosa ya tafsiri niliyoyataja si muhimu mno. Nia yangu ilikuwa ni kuvuta uangalifu wa watafsiri Waswahili, kuwasaidia waelewe zaidi matini ya Kirusi na kuizingatia kwa makini katika kuendeleza kazi yao ya ufasiri yenye maana kubwa. Natumaini kuwa tafsiri hizo zitawasaidia

TAFSIRI MPYA KIRUSI – KISWAHILI

Watanzania wajjulisha na fasihi tajiri ya Kirusi ambayo inaweza kuchangia katika kuelimisha na kuiburudisha jamii ya Waswahili.